

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
CLARIFICATIONS OF 2012 POPULATION AND HOUSING CENSUS QUESTIONS
[ENUMERATORS' MANUAL]

APRIL, 2012

Prepared by:-

National Bureau of Statistics

Ministry of Finance

P. O. Box 796

Dar es Salaam

Phone: +255 22 2122722/3/4,

Fax: +255 22 2130852,

Email: dg@nbs.go.tz,

Website: www.nbs.go.tz

Office of Chief Government Statistician

Revolutionary Government of Zanzibar

President's Office, Finance, Economy and Development Planning

P. O. Box 2321

Zanzibar

Phone: +255 24 2231869,

Fax: +255 24 2231742,

Email: zanstat@zanlink.go.tz,

Website: www.ocggs.go.tz

Table of contents

- 1.0 Foreword
- 2.0 Introduction
- 3.0 General description of census questions
- 4.0 Explanations/clarifications of questions

1.0 Foreword

The clarifications of the 2012 population and housing census questions have been prepared to educate the supervisor or the facilitator on important information about questions that will be asked during census. The questions contained here are the same questions found in the questionnaires that will be used by the census enumerators in interviews.

This enumerators' manual explains step by step all the questions that will be asked during census. Clarifications provided in this manual provide explanations why a particular question is asked and what types of answers are expected from each question asked.

Explanation of these questions will help the government follow-up and evaluate National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (NSGRP) and Zanzibar Strategy for Growth and Reduction of Poverty (ZSGRP), National Development Vision of 2025 for Tanzania mainland and 2020 for Tanzania Zanzibar, the five year Development Plans (2011/12-2015/2016) and the Millennium Development Goals for 2015.

For further clarifications, contact;

Dr. Albina Chuwa
Director General
Office of National Bureau of Statistics
Dar es Salaam

Hajjat Amina Mrisho Said
Census Commissioner

Mohamed Hafidh Rajab
Director General
Office of Director General, Revolutionary Government of Zanzibar

Mwalim Haji Ameir
Census Commissioner

2.0 Introduction

Population and housing census will take place on 26th August, 2012, which will be ten years after the last census was conducted in 2002. Other censuses were conducted in 1967, 1978, and 1988. The exercise of counting people in this census will be carried out within a period not exceeding seven days.

This census has questions not exceeding 62 compared to the 2002 census which had 37 questions; questions included focus on agriculture, Tanzanians living in foreign countries, and more. The objective of these questions is to collect more information which will provide the status of Tanzanians demographically, economically, and socially. There are important questions which are normally asked in every census, and new questions, depending on current and future information needs.

Therefore, in order to ensure that all the citizens understand fully these questions, it is appropriate to print this 2012 population and housing census questionnaire manual. This manual is part of efforts put in place to educate the public about the need to fully participate in the census exercise.

We believe that there will be no challenges in answering questions during census if clarifications provided here are well understood by citizens, and thus we will get more accurate information. Clarifications of these questions also understand the importance of removing fear or doubts amongst some citizens, who due to their cultures, traditions, or other reasons have a different perception towards the population and housing census, a perception that is different from that of the nation, which is to collect information for development purposes of the nation.

3.0 General explanations of census questions

In the 2012 population and housing census, there will be three types of questionnaires which will comprise questions based on the information required to be collected. There will be a **community questionnaire** with five major sections which will be used in all the areas where census is taking place and will be filled in by the census enumerator three days before census day. The community questionnaire will collect information on community services such as schools, hospitals, health centers, markets, financial services, cattle dip [places for washing livestock], sources of water, environment, and events/incidences that occurred in communities in the past one year that were troublesome/disturbing, and catastrophic events that took place in the past five years.

The **short questionnaire** will have 37 questions and the **long questionnaire** will have 62 questions. In areas where the short questionnaire will be use, the long questionnaire will not be used, and in places where the long questionnaire will be used, the short questionnaire will not be used. 70 percent of the census areas will use a short questionnaire and the remaining percentage

will use the long questionnaire. All the questions found in the short questionnaire are also found in the long questionnaire; therefore, these questions will be answered by everyone wherever either questionnaire is used. These questions will ask about the name of the head of the household; names of all the people who slept in the respective house the night before August 26th, 2012, and the relationships of these people to the head of the household.

Other questions that follow ask about sex, age, disability status, marital status, citizenship and place of residence, place where the household member spends most of his/her time, and whether or not the household member has a birth certificate. Other questions will focus on general and reproduction-related death in the household; agricultural questions; number of livestock and fish keeping; education for people with ages of four and above; getting the number of households with at least one household member who has social security fund membership; and Tanzanians who live in foreign countries.

For those who will be asked questions from the **long questionnaire**, they'll be required to answer extra questions which will ask about the following; place of birth, place lived in 2011, whether or not parents are alive, economic activities for people who are five years and above, child-bearing status for women aged 12 and above, and on house characteristics and asset/property ownership.

All these questions aim at meeting the various current and future needs of the nation for planning and implementation purposes of various development programs. Therefore, we ask that everyone needs to understand and pay attention to all the questions so that they can answer them correctly.

Important

It is possible that the night before census day a visitor slept in the house but left before the census enumerator arrived. For the purpose of census taking procedures, such person should be counted in the household where he/she slept a night before census and not where he/she is found after census taking began. For this reason, it is important that the head of the household gets all the answers to all the questions that will be asked before the visitor leaves so that he/she is able to answer all the census questions on behalf of the visitor. The census enumerator will arrive in the area where census will be taking place three days before census day to become familiar with the area as well as prepare residents of the respective area.

4.0 Clarifications of questions

Question 2: Please tell me the names of persons who spent the census night (that is, the night before Sunday 26 August, 2012) in your household, starting with the name of the head of household.

For the purposes of census, a household include persons who normally live and eat together (that is, they cooperate in order to meet their daily needs).

Explanation/clarification of the question

This question wants to know the list of all the people who slept in the respective house on the night before census day – that is, the night of 25th before 26th August 2012, starting with the head of the household.

The head of household is a person responsible for a particular household or a person recognized as the leader by other household members in a particular household.

Answers to this question will enable us get the total number of persons from the whole country, average number of persons in households and the level of poverty in the country.

Question 3: What is the relationship of [NAME] to the head of the household?

Explanation/clarification of the question

This question asks about the relationship of other household members to the head of the household. Relationship can be wife/husband, biological son/daughter, biological father/mother, grandson/daughter, other relative, or other [none related]

Answers to this question will enable the nation to get information which will provide an understanding of the real situation in terms of the level of dependency within households, households headed by females and children, for the purpose of planning development programs and formulation of good policies.

Question 4: Is [NAME] a male or a female?

Explanation/clarification of the question

This question aims to know the sex of every household member.

Answers to this question will facilitate the understanding of population of males and females in every household, village/street, ward/shehia, district, region, and nation.

Question 5: How old are you? How old is [NAME]?

Explanation/clarification of the question

This question aims to get the exact age of a household member. For example, a child who has not yet attained the age of 1 year, will be given "00" years.

Answers to this question will help in planning of development programs. Age is very important information in statistics of people in any nation on this earth. Knowing the correct ages of people

enables the nation to develop strategies for improving services such as health, education, water, community development, and many others.

Questions 6 to 11 aim to get information on the disability status of people in the communities.

Is [NAME] an albino, or has difficulty seeing, hearing, walking or climbing stairs, remembering or concentrating, caring for him/herself such as washing or dressing, has a cleft palate, has spinal befiga, has spinal cord injuries, mental illness, or psoriasis?

Questions description

These questions aim to obtain information about disability status in the communities.

Answers on these questions will enable the nation understand how many people have disabilities and types of disabilities, and thus allow the nation develop sustainable programs for this special group in the community.

Question 12: Is [NAME] currently married, living together, divorced, separated, or spouse died?

For the purposes of census, marriage is when two individuals of opposite sex live together as husband and wife, whether married traditionally, in religious or civil settings.

Explanation/clarification of the question

This question asks about the marital status of every household member; the question wants to know the marital status of household member depending on marriage laws and traditions in Tanzania.

Answers to this question will enable the nation to understand the number of people in the communities who are married and those who are not in order to plan for their special needs. The answers will also help understand at what age people get married for the first time (Age at First Marriage).

Question 13: [NAME] is a citizen of which country?

Explanation/clarification of the question

This question aims to understand the nationality of every person in the community, whether it is by birth or registration.

Answers to this question will enable the nation understand the exact number of citizens of Tanzania, citizens of other countries present on the night before census, and those with two nationalities. The nation will understand the distribution of nationalities in the country.

Questions 14, 16, 17, and 18 asks about household member's place of birth, current place of residence, place lived in 2011, and weather the household member has a birth certificate or birth documentation.

Explanation/clarification of the question

These questions aim to understand how people migrate from one place to another and how towns/cities grow.

Answers to these questions will help the nation understand the amount of people moving from one place to another. Also, these questions will enable the understanding of the amount of growth of towns/cities, and how many people have birth certificates or birth documentations.

Question 15: Where do you, does [NAME] normally spend his/her time during the day?

Explanation/clarification of the question

This question aims to understand where the household member spends most of his/her time during the day. Some people normally live in one place, but works or spends most of their time in another place due to various reasons.

Answers to this question will help the nation improve services provided in towns/cities especially during the day. Answers to this question will also help get the population of people found in towns/cities during the day (day time population).

Question 19: Is [NAME]'s father alive? Is [NAME] mother alive?

Explanation/clarification of the question

This question aims to get information about whether or not the biological parents of a household member are alive.

Answers to this question will help the nation get the population of orphans, as a result, facilitate development of programs and improve policies on orphans.

Questions 20 to 22 ask about education for any person aged 4 years and above.

These questions aim to understand whether the household member can read and write, current or level of education reached, and whether he/she is currently in school or dropped out of school.

Explanation/clarification of the question

Answers to these questions will enable the nation understand the number of people who can read and write, distribution of education levels, and number of people who completed and those who dropped out of school.

Questions 23, 24, 25, 26, and 27 ask about economic activities in the past 24 months and past one week, employments status, work, and main activities at work place (industry) for individuals aged 5 years and above.

For census purposes, a job is any economic activity, whether you get paid, make profit, do barter trade, or for domestic paid jobs.

Explanation/clarification of the question

Questions on economic activities will enable the nation understand the level of employment in various economic sectors, types of employment, scarcity of employment, amount of available labor force, and areas of employment.

Question 28 to 32 aims to understand the fertility trends in our communities, including child born alive but died [i.e., stillbirth and neonatal or perinatal deaths], and children born alive in the past twelve months and whether they're still alive.

Explanation/clarification of the question

The purpose of these questions is to get the fertility rate in the country.

Questions 33 to 40 ask about death and death that resulted from child bearing in the past 12 months. These questions are asked and answered by the head of the household or another person who will respond to these questions on behalf of the household head.

Explanation/clarification of the question

All these questions aim to get death rate, causes of death, including those related to child bearing. The questions will further enable the nation understand the average age of death (life expectancy).

The answers to these questions will enable the nation understand whether there was any death within a household during the period specified.

Questions 41 to 52 ask about the house characteristics and ownership of assets/properties and they are answered by the head of the household.

These questions ask about types of home ownership and materials used for construction of the house household members live in. Also, these questions aim to understand services available in the house, for example, water, toilets, energy source for cooking and lighting the house).

Explanation/clarification of the question

Answers to these questions will enable the nation understand the level of poverty in the households.

Questions 53 to 57 ask about food crops, livestock, and fish keeping.

Question: Is there any member from this household who engaged (or currently) him/herself in farming corn/maize, cassava, banana, or rice during 2011/12 agricultural year, keeping of cows, goats, sheep, chickens, or fish up to the night before census?

Explanation/clarification of the question

These questions aim to know types of major crops grown and number of livestock kept in order to understand the level of food security in the households; to improve agricultural and livestock policies, and to develop a foundation for research in the respective sectors.

Questions 58 to 61 ask about Tanzanians who live in foreign countries.

These questions aim to understand the number of Tanzanians who live in foreign countries and the level of their contribution to the economy of their families in Tanzania and the nation at large during the past twelve months.

Explanation/clarification of the question

The answers to these questions will help steer the discussions on dual citizenship in the right direction during preparation of a new constitution.

Question 62 asks about social security funds for communities.

Is there a person in this household who is a member of any of the following social security funds? National Social Security Fund (NSSF), Zanzibar Social Security Fund (ZSSF), Parastatal Pension Fund (PPF), Public Service Pension Fund (PSPF), Government Employee Provident Fund (GEPF), Local Authority Pension Fund (LAPF), and National Health Insurance Fund/Community Health Fund (NHIF/CHF).

Explanation/clarification of the question

This question aims to know the number of households that have at least one member with social security funds.

Answers to this question will help understand the numbers of households with at least one household member who is a member of social security funds. This information will enable social security funds to expand provision of their services and improve the economies at household level, and consequently reduce poverty.

CENSUS FOR DEVELOPMENT: PREPARE TO BE COUNTED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

UFAFANUZI WA MASWALI YA

SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2012



APRILI, 2012



Kimetayarishwa na:-



Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha
S. L. P 796
Dar es Salaam.

Simu: +255 22 2122722/3/4,
Kinakilishi: +255 22 2130852,
Barua pepe: dg@nbs.go.tz,
Tovuti: www.nbs.go.tz



Ofisi ya Mtakwimu Mkuu
Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na
Mipango ya Maendeleo
S. L. P 2321
Zanzibar.

Simu: +255 24 2231869,
Kinakilishi: +255 24 2231742,
Barua pepe: zanstat@zanlink.go.tz,
Tovuti: www.ocgs.go.tz



Yaliyomo

1.0	Dibaji.....	ii
2.0	Utangulizi	iv
3.0	Maelezo ya Jumla Kuhusu Maswali ya Sensa	vi
4.0	Ufafanuzi wa Maelezo ya Maswali.....	1



1.0 Dibaji

Ufafanuzi huu wa maswali ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 umetayarishwa ili kumuelimisha na kumpatia kiongozi au mhamasishaji maelezo muhimu kuhusu maswali yatakayoulizwa wakati wa Sensa. Maswali haya ndio yaliyomo katika madodoso ambayo atayatumia Karani wa Sensa kuhoji.

Kitabu hiki cha ufafanuzi kinaeleza hatua kwa hatua maswali yote yatakayoulizwa wakati wa Sensa. Ufafanuzi huu umejikita katika kutoa maelezo kwa nini swali husika linaulizwa na nini kinachotarajiwa kutoka majibu ya swali linaloulizwa.

Ufafanuzi wa maswali hayo utasaidia Serikali kufuatilia na kutathmini MKUKUTA na MKUZA, Dira za Taifa za Maendeleo kwa mwaka 2025 Tanzania Bara na mwaka 2020 kwa Tanzania



Zanzibar, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) na Malengo ya Milenia ya mwaka 2015.

Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na;

Dkt. Albina Chuwa

Mkurugenzi Mkuu

Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Dar es Salaam

Mohamed Hafidh Rajab

Mtakwimu Mkuu

Ofisi ya Mtakwimu Serikali

ya Mapinduzi Zanzibar

Hajjat Amina Mrisho Said

Kamishna wa Sensa

Mwalim Haji Ameir

Kamisaa wa Sensa

Aprili, 2012



2.0 Utangulizi

Sensa ya Watu na Makazi itafanyika tarehe 26 Agosti, 2012 ikiwa ni miaka kumi baada ya Sensa ya mwisho iliyofanyika mwaka 2002. Sensa nyingine zilifanyika katika miaka ya 1967, 1978 na 1988. Zoezi la kuhesabu watu katika Sensa hii litadumu kwa muda usiozidi siku saba.

Sensa hii ina maswali yapatayo 62 yakihusisha maswali ya kilimo, Watanzania waishio nje ya nchi na mengineyo ikilinganishwa na Sensa ya mwaka 2002 ambayo ilikuwa na maswali 37. Lengo la maswali haya ni kukusanya takwimu zaidi ambazo zitatoa hali halisi ya Watanzania kidemografia, kiuchumi na kijamii. Yapo maswali ya msingi ambayo huulizwa katika Sensa zote, na maswali mapya kulingana na mahitaji ya kitakwimu ya sasa na miaka ijayo.

Kwa hivyo, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa vyema maswali hayo, imeonekana ni vyema kuchapisha kitabu hiki cha Ufafanuzi wa Maswali ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2012. Kitabu hiki ni sehemu ya jitihada za kuelimisha umma kushiriki kikamilifu katika zoezi la Sensa.

Tunaamini kuwa, ufafanuzi huu ukieleweka vyema kwa wananchi, hakutakuwa na tatizo katika kujibu



maswali wakati wa Sensa hivyo kupata takwimu sahihi. Ufafanuzi huu wa maswali umezingatia pia umuhimu wa kuwatoa hofu au wasiwasi walionao baadhi ya wananchi ambao kutokana na mila, desturi au sababu nyingine wanaiangalia Sensa ya Watu na Makazi katika mtazamo tofauti na ule wa kitaifa ambao ni kukusanya takwimu kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa.



3.0 Maelezo ya Jumla Kuhusu Maswali ya Sensa

Katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kutakuwa na aina tatu za madodoso ambayo yatakuwa na maswali kulingana na aina ya taarifa/takwimu zinazotakiwa kukusanywa. Kutakuwa na **Dodoso la Jamii** lenye sehemu kuu tano litakalotumika kwenye maeneo yote ya kuhesabia watu na litajazwa na Karani wa Sensa siku tatu kabla ya Siku ya Sensa. Dodoso la Jamii litakusanya taarifa kuhusu huduma za jamii kama vile shule, hospitali, vituo vya afya, masoko, huduma za fedha, majosho, vyanzo vya maji, mazingira, matukio yaliyotokea katika jamii katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita ambayo ni kero kwa jamii, na maafa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Dodoso Fupi litakuwa na maswali 37 na **Dodoso Refu** litakuwa na maswali 62. Mahali ambapo Dodoso Fupi litatumika kuhesabu watu Dodoso Refu halitatumika, na pale ambapo Dodoso Refu litatumika Dodoso Fupi halitatumika. Asilimia 70 ya maeneo ya kuhesabia watu yatatumia Dodoso Fupi



na asilimia iliyobaki itatumia Dodoso Refu. Maswali yote ya Dodoso Fupi yamo pia katika Dodoso Refu hivyo maswali hayo yatajibiwa na watu wote popote pale ambapo madodoso haya yatatumika. Maswali hayo yatauliza juu ya jina la mkuu wa kaya; majina ya watu wote waliolala katika kaya hiyo katika usiku wa kuamkia tarehe 26 Agosti, 2012 na uhusiano wa watu hao na mkuu wa kaya.

Maswali mengine yatakayofuata yatataka kujua jinsi, umri, hali ya ulemavu, hali ya ndoa, uraia na mahali anapoishi, na anaposhinda mwanakaya na kama ana cheti cha kuzaliwa. Aidha, yataulizwa maswali juu ya vifo na vifo vitokanavyo na uzazi katika kaya; maswali ya kilimo, idadi ya mifugo na ufugaji wa samaki; elimu kwa watu walio na umri wa miaka minne na zaidi; kupata idadi ya kaya zenye angalau mwanakaya mmoja ambaye ni mwanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamiii na Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

Kwa wale watakaoulizwa maswali kutoka **Dodoso Refu** watatakiwa kujibu maswali ya ziada ambayo yatahusu; mahali alipozaliwa, alipokuwa anaishi mwaka 2011,



uhai wa wazazi, shughuli za kiuchumi kwa watu walio na umri wa miaka mitano na zaidi; hali ya uzazi kwa wanawake wenye umri wa miaka 12 na zaidi; na maswali yanayohusu nyumba na umiliki wa rasilimali.

Maswali yote haya yana lengo la kukidhi mahitaji mbalimbali ambayo Taifa linahitaji hivi sasa na baadaye kwa ajili ya upangaji na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, kila mtu anaombwa ayaelewe na ayazingatie maswali yote haya ili aweze kuyajibu kwa ufasaha.

Muhimu

Inawezekana katika usiku wa kuamkia Siku ya Sensa, mgeni alilala kwenye kaya na akaondoka kabla ya Karani wa Sensa hajafika. Kwa utaratibu wa Sensa mgeni huyo atatakiwa kuhesabiwa hapo alipolala na siyo huko atakapokutwa baada ya Siku ya Sensa. Kwa ajili hiyo, ni vizuri kwa mkuu wa kaya akapata majibu ya maswali yote yatakayoulizwa kabla mgeni huyo hajaondoka ili aweze kuyajibu maswali ya Sensa kwa niaba ya mgeni wake. Karani wa Sensa atafika katika eneo la



**kuhesabia watu siku tatu kabla ya siku ya Sensa
kultambua eneo na kuwaandaa wakazi wa eneo hilo.**



4.0 Ufafanuzi wa Maelezo ya Maswali

SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>Swali la 2: Tafadhali nitajie majina ya watu wote waliolala katika Kaya hii usiku wa kuamkia Siku ya Sensa, yaani usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili ya tarehe 26 Agosti, 2012, ukianza na jina la Mkuu wa Kaya.</p> <p>Kwa madhumuni ya Sensa Kaya ni jumla ya watu ambao kwa kawaida huishi pamoja na kula pamoja (yaani hushirikiana katika kupata mahitaji yao ya</p>	<p>Swali hili linataka kujua orodha ya watu wote waliolala katika kaya husika usiku wa kuamkia Siku ya Sensa yaani tarehe 25 kuamkia tarehe 26 Agosti, 2012 kwa kuanzia na Mkuu wa Kaya.</p> <p>Mkuu wa Kaya ni yule mtu anayewajibika kwa Kaya hiyo au yule ambaye anatambuliwa na wanakaya kama kiongozi wa Kaya hiyo.</p> <p>Majibu ya Swali hili yatatuwezesha kupata idadi ya watu wote nchini, wastani wa idadi ya watu katika</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
kila siku).	Kaya na kiwango cha umaskini nchini.
Swali la 3: Je, [JINA] una/ana uhusiano gani na Mkuu wa Kaya?	<p>Swali hili linauliza uhusiano wa wanakaya wengine na Mkuu wa Kaya. Uhusiano huo unaweza kuwa ni; Mke/Mume, Mtoto wa Kiume/Kike, Baba/Mama Mzazi, Mjukuu, Ndugu Mwingine, au Mtu Mwingine.</p> <p>Majibu ya swali hili yataliwezesha Taifa kupata takwimu zitakazotoa hali halisi ya kiwango cha utegemezi ndani ya Kaya, Kaya zinazoongozwa na wanawake, na watoto kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo na kutunga sera</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
	stahiki.
Swali la 4: Je, [JINA] ni wa kiume au wa kike?	<p>Swali hili linataka kujua jinsi ya kila mtu.</p> <p>Majibu ya swali hili yatatuwezesha kujua idadi ya wanaume na wanawake katika kila Kaya, Kijiji/Mtaa, Kata/Shehia, Wilaya, Mkoa na Taifa.</p>
Swali la 5: Je, [JINA] una/ana umri wa miaka mingapi?	<p>Swali hili linakusudia kupata umri kamili wa mwanakaya. Kwa mfano mtoto ambaye hajafikia umri wa mwaka mmoja atawekewa umri sifuri “00”.</p> <p>Majibu ya swali hili yatasaidia katika kupanga mipango ya maendeleo. Umri ni taarifa muhimu sana</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
	<p>katika takwimu za watu kwenye Taifa lolote lile hapa duniani. Kwa kujua takwimu sahihi za umri, Taifa litaweza kupanga mipango yake ya kuboresha afya, elimu, maji, maendeleo ya jamii na mengine mengi.</p>
<p>Swali la 6 hadi la 11 yanalenga kupata taarifa za hali ya ulemavu katika jamii.</p> <p>Je, [JINA] ni albino au ana matatizo ya kuona, kusikia, kutembea au kupanda ngazi, kukumbuka au kufanya</p>	<p>Maswali haya yanalenga kupata taarifa za hali ya ulemavu katika jamii.</p> <p>Majibu ya maswali haya yatawezesha Taifa kujua idadi ya watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali ili kuliwezesha Taifa kuweka mipango endelevu kwa kundi hilo maalum katika jamii.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>kitu kwa umakini, kujihudumia kama vile kuoga au kuvaa nguo, Mdomo kasuku/mpasuko wa mdomo; Kichwa kikubwa na mgongo wazi; uti wa mgongo; afya ya akili, au ulemavu wa mabakamabaka ya ngozi?</p>	
<p>Swali la 12: Je, [JINA], kwa hivi sasa Hajaoa/Hajaolewa, Ameoa/Ameolewa; Wanaishi Pamoja, Ameachana, Ametengana, au amefiwa na Mke/Mume?</p> <p>Kwa madhumuni ya Sensa ndoa ni watu</p>	<p>Swali hili linahusu hali ya ndoa ya kila mwanakaya; linataka kujua hali ya ndoa ya mwanakaya kulingana na sheria za ndoa na desturi za Tanzania.</p> <p>Majibu ya swali hili yataliwezesha Taifa kujua idadi ya watu katika jamii wenye ndoa na wale wasio</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
wawili wenye jinsi tofauti wanaoishi pamoja kama mume na mke ikiwa wameoana kimila, kidini au kiserikali.	na ndoa kwa ajili ya kuwapangia mahitaji yao maalum. Majibu yatasaidia pia kujua umri wa kuoa na kuolewa mara ya kwanza (Age at First Marriage).
Swali la 13: Je, [JINA] ni raia wa nchi gani?	<p>Swali hili linalenga kujua uraia wa kila mtu katika jamii iwe kwa kuzaliwa au kwa kuandikishwa.</p> <p>Majibu ya swali hili yataliwezesha Taifa kujua idadi kamili ya raia wa Tanzania, raia wa nchi nyingine watakaokuwepo usiku wa kuamkia Siku ya Sensa, na wale wenye uraia wa nchi mbili. Taifa litaweza kujua mchanganuo wa uraia nchini.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>Maswali ya 14, 16, 17 na 18 yanauliza kuhusu mahali alipozaliwa mwanakaya, anapoishi, alipoishi mwaka 2011 na kama ana cheti cha kuzaliwa au tangazo.</p>	<p>Maswali haya yanalenga kufahamu namna watu wanavyohama na kuhamia kutoka sehemu moja hadi nyingine na kutambua ukuaji wa miji.</p> <p>Majibu ya maswali haya yatalisaidia Taifa kujua kiwango cha watu wanavyohama na kuhamia kutoka sehemu moja hadi nyingine. Pia, yatawezesha kujua kiwango cha ukuaji wa miji na wangapi wana vyeti vya kuzaliwa au tangazo.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>Swali la 15: Je, kwa kawaida [JINA] huwa unashinda/anashinda wapi?</p>	<p>Swali hili linataka kujua mahali ambapo mwanakaya anashinda au anapotumia muda wake mwingi wakati wa mchana. Baadhi ya watu kwa kawaida huishi sehemu moja na kufanya kazi au hushinda sehemu nyingine kwa sababu mbalimbali.</p> <p>Majibu ya swali hili yatalisaidia Taifa kuboresha huduma katika maeneo ya mijini hasa nyakati za mchana. Majibu yatasaidia kupata idadi ya watu walioko mijini wakati wa mchana (Day Time Population).</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>Swali la 19: Je, baba mzazi wa [JINA] yu hai? Je, mama mzazi wa [JINA] yu hai?</p>	<p>Swali hili linalenga kupata taarifa juu ya uhai wa wazazi halisi (wa kibaiolojia).</p> <p>Majibu ya swali hili yatalisaidia Taifa kupata idadi ya watoto yatima na hivyo kuliwezesha kupanga mipango na kuboresha sera inayohusu watoto yatima.</p>
<p>Swali la 20 hadi la 22 yanahusu Elimu kwa watu wenye miaka 4 na zaidi.</p> <p>Maswali haya yanalenga kujua iwapo mwanakaya anajua kusoma na kuandika, kiwango cha elimu alichopo au alichofikia, anasoma au</p>	<p>Majibu ya maswali haya yataliwezesha Taifa kujua idadi ya watu wanaojua kusoma na kuandika, viwango vya elimu, waliomaliza na walioacha shule.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
ameacha shule.	
<p>Maswali ya 23, 24, 25, 26 na 27 yanahusu shughuli za kiuchumi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, na wiki moja iliyopita, hali ya ajira, kazi na shughuli kuu mahali pa kazi kwa watu wenye umri wa miaka 5 na zaidi.</p> <p>Kwa madhumuni ya Sensa, kazi ni shughuli yoyote ile ya kiuchumi, iwe ya kulipwa, ya kupata faida, kubadilishana bidhaa au shughuli za nyumbani za malipo.</p>	<p>Majibu ya maswali haya ya shughuli za kichumi yataliwezesha Taifa kujua kiwango cha ajira katika sekta mbalimbali za uchumi, aina ya ajira, ukosefu wa ajira, nguvu kazi ya Taifa na sehemu walikoajiriwa au walikoajiri.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
Swali la 28 hadi la 32 yanalenga kujua mwenendo wa uzazi katika jamii yetu ikijumuisha watoto waliozaliwa hai, waliofariki na waliozaliwa hai katika kipindi cha miezi kumi na mbili iliyopita na kama bado wako hai.	Maswali haya yanalenga kupata kiwango cha uzazi nchini.
Swali la 33 hadi la 40 yanahusu vifo na vifo vitokanavyo na uzazi vilivyotokea katika Kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na yanaulizwa na kujibiwa na Mkuu wa Kaya au mtu mwingine ambaye atajibu maswali haya	Maswali yote haya yanalenga kupata kiwango cha vifo, sababu za vifo vikiwemo vitokanavyo na uzazi. Halikadhalika yatawezesha Taifa kupata wastani wa umri wa kuishi (Life Expectancy).



SWALI	MAELEZO/UFAPANUZI
kwa niaba ya Mkuu wa Kaya.	Majibu ya maswali haya yatawezesha Taifa kupata taarifa kama kulitokea kifo/vifo katika Kaya katika kipindi husika.
<p>Swali la 41 hadi la 52 yanahusu nyumba na umiliki wa vifaa na yanajibiwa na Mkuu wa Kaya.</p> <p>Maswali haya yanahusu aina ya umiliki wa nyumba wanayoishi wanakaya na vifaa vilivyotumika katika ujenzi wa nyumba hiyo. Pia, yanalenga kupata huduma zilizopo katika Kaya kama vile; maji, choo, nishati</p>	Majibu ya maswali haya yataliwezesha Taifa kujua kiwango cha umaskini katika Kaya.



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
inayotumika kwa kupikia, na kuangazia.	
<p>Swali la 53 hadi la 57 yanahusu Kilimo cha mazao ya chakula, Mifugo na Ufugaji wa samaki.</p> <p>Swali: Je kuna mwanakaya yeyote katika Kaya aliye/anayejishughulisha na kilimo cha mahindi, muhogo, ndizi au mpunga msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012, ufugaji wa ng'ombe, mbuzi,</p>	<p>Maswali haya yanalenga kufahamu aina ya mazao makuu yanayolimwa na idadi ya mifugo inayofugwa ili kufahamu hali ya usalama wa chakula katika Kaya; kuboresha sera za kilimo na ufugaji, na kuweka msingi kwa tafiti nyingine katika sekta husika.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
kondoo, kuku au ufugaji wa samaki hadi kufikia usiku wa kuamkia Siku ya Sensa?	
<p>Swali la 58 hadi la 61 yanahusu Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania.</p> <p>Maswali haya yanalenga kujua idadi ya Watanzania waishio nje ya nchi na kutambua michango wanayotoa kwa familia zao na Taifa kwa ujumla katika kipindi cha miezi 12 iliyopita</p>	<p>Majibu ya maswali haya yataboresha mjadala wa uraia wa nchi mbili wakati wa mchakato wa kuandaa Katiba mpya.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
<p>Swali la 62 linahusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.</p> <p>Je kuna mwanakaya yeyote ambaye ni mwanachama wa mfuko wa hifadhi ya jamii kati ya ifuatayo? Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Akiba wa</p>	<p>Swali hili linataka kujua idadi ya Kaya ambazo angalau zina mwanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii iliyotajwa.</p> <p>Majibu ya swali hili yatasaidia kupata idadi ya Kaya zenye angalau mwanakaya mmoja ambaye ni mwanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Taarifa hizi zitawezesha Mifuko hiyo kupanua huduma zake na kuongeza uwezo wa uchumi katika ngazi ya Kaya na hatimaye kupunguza umaskini.</p>



SWALI	MAELEZO/UFAFANUZI
Wafanyakazi Serikalini (GEPF), Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya-(NHIF/CHF).	

***SENSA KWA MAENDELEO: JIANDAE
KUHESABIWA***